CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

(UDOM SACCOS LTD)

NAMBARI YA USAJILI:

PRI-DOM-DOM-CC-2022-130

SERA YA UHAMASISHAJI HISA, AKIBA NA AMANA

Imeandaliwa na:
S.L.P 2765, DODOMA
Email:udomsaccosltd@gmail.com
Bodi ya UDOM SACCOS LTD

TOLEO LA 1 , 2025

1. UTANGULIZI 1

1.1. Madhumuni ya Chama 1

1.2. Umuhimu wa Akiba na Amana kwa maendeleo ya kiuchumi ya wanachama na chama. 1

1.3. Changamoto zilizopo katika uwekaji wa Akiba na Amana. 1

SEHEMU YA PILI 4

2. MAANA YA MANENO 4

SEHEMU YA TATU 6

3. TARATIBU ZA UWEKAJI NA UCHUKUAJI WA HISA ZA LAZIMA, HISA ZA HIARI,AKIBA NA AMANA 6

3.1. UWEKEZAJI WA HISA ZA LAZIMA 6

3.2. UWEKAJI WA HISA ZA HIARI 6

3.3. UWEKAJI WA AKIBA 7

3.4. UWEKAJI WA AMANA 8

SEHEMU YA NNE 9

4. MISINGI YA LAZIMA YA KISHERIA KATIKA SERA YA UHAMASISHAJI WA HISA, AKIBA NA AMANA 9

4.1. MASHARTI YA KUFUNGUA, UENDESHAJI NA KUFUNGA AKAUNTI. 9

4.2.UDOM SACCOS ITAFUNGA AKAUNTI YA MWANACHAMA ENDAPO 9

SEHEMU YA TANO 10

5. MASHARTI YA UANACHAMA NA KUTOA HISA ZA HIARI NA AMANA 10

SEHEMU YA SITA 11

6. UTARATIBU WA UENDESHAJI WA AKAUNTI MFU 11

7. HITIMISHO 12

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Sera hii imeweka mwongozo wa kisheria na uwazi katika kuweka mikakati ya uhamasishaji wa akiba, Amana na Hisa kwa wanachama wa UDOM SACCOS kwa lengo la kuimarisha mtaji wa chama kwa kuzingatia Sheria ya huduma ndogo za fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2019.

1.1. Madhumuni ya Chama

Madhumuni ya UDOM SACCOS ni kuinua na kuimarisha hali ya wanachama kwa kujijengea utamaduni wa kuweka mara kwa mara akiba, amana na hisa za hiari kwa ajili ya kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii katika siku za mbeleni.
Ili kufikia lengo hilo Chama kitafanya shughuli zifuatazo: -

a. Kupokea Akiba, Amana, Hisa za lazima na hiari za wanachama na kuzihifadhi kwa njia rahisi na salama
b. Kutoa mikopo ya huduma za kijamii na kiuzalishaji yenye masharti nafuu.
c. Kuelimisha wanachama kujijengea tabia ya kuweka Akiba, Amana Hisa za hiari na kutumia kwa malengo mikopo watakayokopeshwa na Chama wakati wote.
d. Kutoa faida juu ya Akiba, Amana na Hisa za wanachama baada ya makubaliano ya Mkutano Mkuu.

1.2. Umuhimu wa Akiba na Amana kwa maendeleo ya kiuchumi ya wanachama na chama.

Akiba na Amana husaidia chama cha ushirika kuondoa utegemezi mkubwa wa mikopo ya nje, ndio maana uongozi wa UDOM SACCOS umekuwa ukiwasisitiza wanachama kuongeza kiwango cha uwekaji wa Akiba na Amana ili kukuza uwezo wa ndani wa kifedha kwa chama na mwanachama mmoja mmoja.

1.3. Changamoto zilizopo katika uwekaji wa Akiba na Amana.

1.3.1 Kukosekana kwa mtaji wa ndani

Chama cha ushirika wa akiba na mikopo Chuo Kikuu cha Dodoma kinategemea akiba na amana za wanachama kama chanzo kikuu cha mtaji wake wa ndani. Endapo wanachama hawatachangia akiba na amana ya kutosha, chama kitashindwa kujijengea mtaji wa kutosha, jambo litakalozuia shughuli nyingi za maendeleo kufanyika ndani ya chama.

1.3.2 Kushindwa kutoa mikopo kwa wanachama

Moja ya huduma kuu ya Chama cha ushirika wa akiba na mikopo Chuo Kikuu cha Dodoma ni kutoa mikopo nafuu kwa wanachama wake. Kukosekana kwa amana na akiba toshelevu kunapunguza uwezo wa chama kutoa mikopo, hali

inayowakatisha tamaa wanachama na kuwafanya washindwe kuona faida ya uanachama wao.

1.3.3 Migogoro kati ya wanachama na uongozi

Kukosekana kwa ukwasi wa kutosha huchochea migongano, kwani wanachama wenye uhitaji wa huduma (hasa mikopo) hushindwa kupata wanachohitaji, na mara nyingine huwalaumu viongozi wa chama kwa kushindwa kuwahudumia.

1.3.4 Kutegemea misaada au mikopo ya nje

Kukosekana kwa amana na akiba ya kutosha kwa vyama vya ushirika huvipelekea vyama vya ushirika kutegemea vyanzo vya nje, kama vile taasisi za kifedha au mashirika ya misaada. Hali hii huongeza utegemezi na kuvifanya vyama kutojiendesha kiushindani.

1.3.5 Kupungua kwa imani ya wanachama

Wanachama wanaposhindwa kuona manufaa kutokana na chama kwa sababu hakuna amana na akiba ya kutosha kuendesha shughuli zake, huanza kukosa imani. Hali hii inaweza kupelekea baadhi yao kujiondoa kabisa katika chama.

1.3.6 Kukosa gawio na faida za pamoja

Akiba na amana zinapowekezwa huzaa faida ambazo hugawanywa kwa wanachama kama gawio. Chama kisipokuwa na akiba pamoja na amana hakitaweza kupata faida, hivyo wanachama hukosa gawio na motisha ya kuendelea kushiriki ipasavyo katika chama.

1.3.7 Hatari ya chama kufutwa au kufa

Chama cha ushirika kinaposhindwa kujitegemeza kifedha kutokana na ukosefu wa mtaji, hujikuta kikiwa dhaifu, hali inayoweza kukipeleka kufutwa kisheria au kufa kabisa kwa kukosa uendelevu.

1.3.8 Kukosa uwezo wa kukabiliana na dharura

Vyama vya ushirika vinapokuwa na akiba Pamoja na amana ya kutosha vinaweza kuwasaidia wanachama wake pale wanapokumbwa na changamoto za kifedha au dharura. Kukosekana kwa fedha hizo kunawafanya wanachama wakose msaada wa haraka kutoka kwenye chama.

2. Malengo ya Sera

2.1 Kuongeza kiwango cha akiba na amana za wanachama.

2.2 Kujenga uwezo wa UDOM SACCOS katika usimamizi wa uwekaji na utoaji wa akiba na amana.
2.3 Kuhamasisha nidhamu ya kifedha miongoni mwa wanachama.
2.4 Kukuza uwekezaji wa akiba na amana kwa maendeleo ya pamoja.

3. **Mikakati ya Uhamasishaji**

3.1 Elimu na mafunzo ya kifedha kwa wanachama.
3.2 Kampeni za uhamasishaji (vipeperushi, semina, mikutano).
3.3 Utoaji wa motisha (mf. Zawadi ya fedha au cheti cha pongezi kwa wachangiaji wazuri wa akiba/amana).
3.4 Ubunifu wa mifumo ya kidigitali ili kurahisisha uwekaji akiba/amana.
3.5 Ushirikiano na taasisi za fedha kuongeza thamani ya akiba/amana.

SEHEMU YA PILI

2. MAANA YA MANENO

i. **KIINGILIO**

Kiingilio ni fedha anayotoa mwanachama ili kujiunga na Chama. Fedha hii ni pato la Chama, hivyo siyo fedha ya mwanachama. Mwanachama anapoacha au kuachishwa uanachama hatorudishiwa kiasi cha kiingilio alicholipa. Kiingilio kwa sasa ni Tsh 100,000/= (Shilingi Laki moja tu)

ii. **HISA ZA LAZIMA**

Hisa za Lazima ni fedha anayowekeza Mwanachama anapojiunga na kuendelea kuchangia mtaji wa ndani wa Chama na ni moja ya kigezo kikubwa kinachomwezesha kuwa mwanachama halali katika chama na hazitatumika kama dhamana ya mkopo. Hisa za lazima kwa sasa ni mafungu 100 (Kila fungu ni Tsh 10,000/=). Hivyo kila mwanachama anapaswa kutimiza kiasi cha Tsh 1,000,000/= (Shilingi milioni moja tu) ili kuwa mwanachama kamili

Mwanachama hatopewa mkopo endapo hajakamilisha mafungu 100 ya hisa za lazima.

Kiwango cha hisa za lazima kinaweza kubadilika kila mwaka kulingana na maamuzi ya mkutano mkuu wa wanachama kwa lengo la kujenga mtaji wa ndani wa chama.

Hisa za lazima zitakuwa na gawio kila mwaka endapo chama kitapata faida kulingana na mapendekezo ya Bodi ya chama na kuamuliwa na Mkutano Mkuu wa Wanachama.

Aidha, hisa za lazima atapewa mwanachama pindi anapoacha au kuachishwa uanachama na kupewa haki zake ndani ya siku sitini.

iii. **HISA ZA HIARI**

Hisa za hiari ni fedha anayowekeza mwanachama chamani kwa kuendelea kukuza mtaji wa ndani wa Chama na kuweza kutumika kama dhamana ya mkopo na zinaweza kuchukuliwa wakati wowote kama hisa hizo za hiari hazijadhamini mkopo.
Hisa za hiari zitakuwa na gawio mwisho wa mwaka endapo mkutano mkuu utapitisha na kuidhinishwa na Mrajis msaidizi.

iv. **AKIBA**

Akiba ni fedha ambayo Mwanachama huweka katika Chama na hivyo inatumika kujenga mtaji wa ndani wa Chama kwa kukopeshana na Mwanachama anatumia akiba kama dhamana na kigezo kikubwa cha kupata mkopo katika Chama.

Akiba zitakuwa na riba ya 4% (itazidishwa na wastani wa akiba za mwanachama kwa mwaka) kwa mwaka na mabadiliko ya riba yatapendekezwa na Bodi ya chama na kuamuliwa na Mkutano Mkuu. Aidha, akiba atapewa mwanachama pindi tu anapoacha au kuachishwa uanachama na kupewa haki zake ndani ya siku sitini.

v. **AMANA**

Amana ni fedha ambayo Mwanachama huweka katika Chama na hivyo inatumika kujenga mtaji wa ndani wa Chama kwa kukopeshana na Mwanachama anawezakutumia amana kama dhamana ya mkopo japo kiasi kilicho Dhamini mkopo hakioaswi kutolewa hadi mkopo uishe.

Amana zitakuwa na riba ya 4% (itazidishwa na wastani wa amana za mwanachama kwa mwaka) kwa mwaka na mabadiliko ya riba yatapendekezwa na Bodi ya chama na kuamuliwa na Mkutano Mkuu. Aidha, amana atapewa mwanachama wakati wowote kama fedha hizo hazitakuwa zimetumika kama dhamana ya mkopo.

SEHEMU YA TATU

3. TARATIBU ZA UWEKAJI NA UCHUKUAJI WA HISA ZA LAZIMA, HISA ZA HIARI, AKIBA NA AMANA

Pamoja na maelezo yaliyotolewa katika sehemu ya pili, utaratibu wa uwekaji na uchukuaji wa hisa za lazima, hisa za hiari, akiba na amana katika UDOM SACCOS utakuwa kama ifuatavyo;

3.1. UWEKEZAJI WA HISA ZA LAZIMA

Hisa za lazima ni fedha anayopaswa kuweka mwanachama anapojiunga na kuendelea kuchangia mtaji wa ndani wa Chama na ni moja ya kigezo kikubwa kinachomwezesha kuwa mwanachama halali katika chama.

Hisa za lazima zitakuwa na utaratibu ufuatao;

(i) Thamani ya Hisa moja kwa sasa ni Tshs. 10,000/=.
(ii) Mwanachama anatakiwa awe na kiasi cha hisa 100 ili aweze kukopa.
(iii) Hisa za lazima hazitatumika kama dhamana ya mkopo
(iv) Hisa za lazima hazitaruhusiwa kupunguzwa kwa hali yoyote ile.
(v) Mwanachama anayetaka kujitoa anaruhusiwa kuchukua hisa zake zote kwa kutoa taarifa ya siku sitini kabla ya malipo halisi, ili kuwezesha Chama kupata muda wa kuziuza kwa wengine.

N.B: Utaratibu huu haukatazi mwanachama mwenye uwezo wa kununua hisa Kwa mkupuo zaidi ya ilivyoelekezwa hapo juu, ilimradi isizidi asilimia 20% ya hisa zote Chamani.

3.2. UWEKAJI WA HISA ZA HIARI

Hisa za hiari ni fedha anayowekeza mwanachama chamani kwa lengo la kuendelea kukuza mtaji wa ndani wa Chama kwa kujenga utamaduni wa kujiwekea hisa kwa hiari ili kukuza mtaji wa chama na mwanchama.

Hisa za hiari zitakuwa na utaratibu ufuatao:

i. Zinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo
ii. Zinaweza kuchukuliwa wakati wowote Kama hisa hizo za hiari hazijadhamini mkopo.

iii. Hisa za hiari zitakuwa na riba juu ya hisa za hiari **6%** kwa mwaka na mabadiliko ya riba yatapendekezwa na Bodi ya chama na kuamuliwa na Mkutano Mkuu wa Wanachama.

iv. Hakuna kiasi cha mwisho kwa Mwanachama kujiwekea hisa za hiari ili mradi kiasi hicho hakitaruhusiwa kuzidi zaidi ya $^1/_5$ au asilimia 20% ya hisa za hiari zote za Wanachama.

v. Kiasi cha hisa za hiari kilichowekwa kama dhamana ya mkopo kwa Mwanachama aliyekopa au kiasi alichomdhamini mwanachama mwingine, kiasi hicho hakitatumika tena kudhamini/kujidhamini kuchukua mkopo mwingine.

vi. Hisa za hiari atapewa mwanachama pindi anapoacha au kuachishwa uanachama na kupewa haki zake ndani ya siku sitini.

3.3. UWEKAJI WA AKIBA

Kila mwanachama anatakiwa kuweka Akiba mara kwa mara kwa ajili ya kutunisha mtaji wa Chama na mwanachama mwenyewe.

i. Akiba ni kigezo kikubwa na muhimu katika kumkopesha mwanachama.

ii. Kila mwanachama anayejiunga na Chama atatakiwa kuweka Akiba na ndiyo itakayotumika kumwezesha kupata mkopo si zaidi ya mara tatu (3) ya kiasi cha akiba zake Chamani.

iii. Kila mwanachama anatakiwa awe na Akiba si chini ya Tshs 500,000/= katika akaunti yake, kiasi hichi hakitoruhusiwa kukitoa wakati wote labda kama amejitoa au kutolewa uanachama. Mwanachama anaruhusiwa kuweka akiba zaidi wakati wowote.

iv. Kiasi cha Akiba kilichowekwa kama dhamana ya mkopo kwa Mwanachama aliyekopa au kiasi alichomdhamini mwanachama mwingine, kiasi hicho hakitatumika tena kudhamini/kujidhamini kuchukua mkopo mwingine.

v. Kwa kuwa Akiba ndiyo dhamana na kigezo cha kupata mkopo hivyo kiasi cha Akiba kilichowekwa kama dhamana hakitaruhusiwa kupunguzwa au kuchukuliwa mpaka mkopo uliodhaminiwa umerejeshwa wote.

vi. Mwanachama anayejitoa Chamani, atatakiwa atoe taarifa ndani ya siku 60 ili achukue akiba zake na haki zake zingine.

vii. Adhabu ya kuchelewesha akiba katika chama ni asilimia 5% kwa mwezi. (Kwa kiwango cha akiba ya lazima)

viii. Mwanachama atahesabiwa amechelewesha Akiba endapo hatolipa ndani ya siku 30 za mwezi husika.

ix. Mwanachama anapaswa kuchangia kiasi kisichopungua Tsh 20,000/= kila mwezi kama akiba. Mwanachama anaruhusiwa kuchangia zaidi ya kiwango cha akiba ya lazima iliyo pangwa.

3.4. UWEKAJI WA AMANA

Kila mwanachama anatakiwa kuweka Amana mara kwa mara kwa ajili ya kutunisha mtaji wa Chama na mwanachama mwenyewe.

x. Amana si kigezo kikubwa na muhimu katika kumkopesha mwanachama, japo inaweza kutumika kama dhamana mbadala pindi mwanachama anapokuwa hana akiba ya kutosha pindi anapoomba mkopo

xi. Kiasi cha Amana kilichowekwa kama dhamana ya mkopo kwa Mwanachama aliyekopa au kiasi alichomdhamini mwanachama mwingine, kiasi hicho hakitatumika tena kudhamini/kujidhamini kuchukua mkopo mwingine.

xii. Kama Amana itatumika kama dhamana ya mkopo kiasi hicho kilichotumika kama dhamana hakitaruhusiwa kupunguzwa au kuchukuliwa mpaka mkopo uliodhaminiwa umerejeshwa wote.

xiii. Mwanachama anayejitoa Chamani, atatakiwa atoe taarifa ndani ya siku 60 ili achukue amana zake na haki zake zingine.

xiv. Adhabu ya kucheleweshaamana katika chama ni asilimia 5% kwa mwezi. (Kwa kiwango cha amana ya lazima)

xv. Mwanachama atahesabiwa amecheleweshaAmana endapo hatolipa ndani ya siku 30 za mwezi husika.

xvi. Mwanachama anapaswa kuchangia kiasi kisichopungua Tsh 30,000/= kila mwezi kama amana. Mwanachama anaruhusiwa kuchangia zaidi ya kiwango cha amana ya lazima iliyo pangwa.

SEHEMU YA NNE

4. MISINGI YA LAZIMA YA KISHERIA KATIKA SERA YA UHAMASISHAJI WA HISA, AKIBA NA AMANA

4.1. MASHARTI YA KUFUNGUA, UENDESHAJI NA KUFUNGA AKAUNTI.

(i) UDOM SACCOS itakuwa na masharti na vigezo vya kufungua akaunti kwa kila mwanachama ambazo zitahusisha miamala ya Hisa, Akiba na Amana.

(ii) Miamala ya Akaunti hizi itaonekana katika leja kadi ya mwanachama na kitabu cha mwanachama.

(iii) Wakati wote mwanachama anatakiwa kufanya malinganisho kati ya kitabu cha mwanachama (pass book) na leja kadi yake iliyoko chamani.

4.2. UDOM SACCOS ITAFUNGA AKAUNTI YA MWANACHAMA ENDAPO

(i) Mwanachama husika amehiari kujiondoa katika uanachama wake ndani ya UDOM SACCOS

(ii) Mwanachama amefariki

SEHEMU YA TANO

5. MASHARTI YA UANACHAMA NA KUTOA HISA ZA HIARI NA AMANA

i. Hisa za Hiari na Amana za mwanachama zinaweza kuchukuliwa wakati wowote isipokuwa kama Hisa hizo za Hiari au Amana hizo hazijatumika kama dhamana ya mkopo wa mwanachama husika.

ii. Endapo mwanachama wa UDOM SACCOS anataka kutoa aidha Hisa za Hiari au Amana atatakiwa kutoa taarifa kwa maandishi akieleza kusudio lake la kutoa kiasi hicho cha fedha.

iii. Kulingana na vipengele tajwa hapo juu (5. i na 5.ii) akaunti ya mwanachama haitaruhusiwa kutoa fedha hizo kama akaunti hizo hazina fedha zinazolingana na kiasi kinachotaka kutolewa.

SEHEMU YA SITA

6. UTARATIBU WA UENDESHAJI WA AKAUNTI MFU

i. UDOM SACCOS itaitambua akaunti yoyote kuwa akaunti mfu endapo akaunti hiyo itakuwa haina miamala iliyofanyika kwa kipindi cha mwaka mmoja.

ii. UDOM SACCOS itafuta akaunti MFU iwapo mwanachama au mrithi wake (muwakilishi wake kisheria**)** hatafanya mawasiliano kimaandishi na chama ndani ya miaka mitano.

iii. Fedha hizo kulingana na 6.ii hapo juu, UDOM SACCOS itatoa siku tisini ya maandishi kumtaarifu mwanachama huyo MFU au mrithi wake kwamba, akaunti yake itafungwa na fedha hizo zitahamishiwa kwenye UDOM SACCOS ‘’Reserve Fund Account’’.

iv. Endapo mwanachama au mrithi wake, hajafika chamani, Bodi ya chama kwa idhini ya mkutano mkuu itahamishia fedha hizo kwenye UDOM SACCOS ‘’Reserve Fund Account’’ na mwanachama au mrithi wake atajulishwa kwa maandishi juu ya hatua hizo zilizochukuliwa kwa anwani yake inayojulikana.

v. Endapo mwanachama MFU atarudi na kuwasiliana na UDOM SACCOS kuhusu Akaunti yake – MFU, UDOM SACCOS itarudisha fedha hizo kwenye akaunti yake na kurudisha fedha zake za awali yaani fedha za tangu akaunti yake ilipofungwa au ilipotambuliwa kuwa MFU.

7. HITIMISHO

Sera hii itafanyiwa maboresho (marekebisho) mara kwa mara ili kurekebisha, kuongeza jambo pale itakapoonekana kuwa inalazimu kufanya hivyo kwa maslahi ya wanachama kadiri Bodi na Mkutano Mkuu itakavyoona inafaa. Maboresho yoyote yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018 na Kanuni ya huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Sera hii ya uhamasishaji wa Hisa, Akiba na Amana imeandaliwa na Bodi ya UDOM SACCOS na kuthibitishwa na mkutano mkuu wa wanachama uliofanyika tarehe _____

Mrajis wa Vyama vya Ushirika

Tarehe_____